



Royal Commission
into Aged Care Quality and Safety

SWAHILI

Tume ya Kifalme kuchunguza Ubora na Usalama wa Utunzaji wa Wazee (The Royal Commission into Aged Care Quality and Safety)

Tume ya Kifalme kuchunguza Ubora na Usalama wa Utunzaji wa Wazee imeanzishwa kuangalia ubora wa huduma za utunzaji wa wazee na kama huduma hizo zinatosheshekeza mahitaji ya jamii ya Australia. Hayo ni pamoja na:

- Kuwatunza wazee wanaoishi nyumbani
- Watu wanaoishi na ugonjwa wa shida ya akili, na
- Watu wanaoishi katika makazi ya utunzaji wa wazee pamoja na watu wa umri chini zaidi wenye ulemavu.

Tume itachunguza utunzaji unaotolewa mijini, pamoja na maeneo ya kikanda na kijijini. Itaangalia jinsi ya huduma za utunzaji wa wazee zinaweza kuboresha baadaye.

Tume inataka kusikia uzoefu wako, wote mzuri na mbaya. Pia inataka madokezo yako kwa njia za kuboresha mfumo wa utunzaji wa wazee. Waweza kuambia hadithi yako kwa Tume kwa:

- Kupiga simu: 1800 960 711 (kati ya saa 2:00 asubuhi hadi saa 2:00 jioni [8:00am-8:00pm AEDT] Jumatatu - Ijumaa ila kwa likizo za umma). Huduma za ukalimani zinapatikana.
- kuandikia: GPO Box 1151, Adelaide SA 5001 (tutatafsiri barua yako)
- Kujaza fomu ya mtandaoni kwa:
<https://agedcare.royalcommission.gov.au/submissions/Pages/default.aspx>
- Kupeleka baruapepe: ACRCenquiries@royalcommission.gov.au

Ukiwa na shida na huduma ya utunzaji wa wazee inayohitaji tendo la mara moja.

Tume ya Kifalme haiwezi kutatua migogoro ya mtu binafsi au malalamiko. Haiwezi kuamuru mtoaaji wa utunzaji au mtu kufanya tendo fulani au kulipa fidia. Hata hivyo, Tume ya Ubora na Usalama wa Utunzaji wa Wazee inawezakana kusaidia katika hali hii kwa sababu Tume ni shirika la malalamiko kwa huduma za utunzaji wa wazee zinazotolewa ruzuku na Serikali ya Australia.

Ikiwa ukitaka kutoa lalamiko kuhusu ubora wa huduma za utunzaji wa wazee zinazotoa kwa mtu sasa hivi, unaweza kuwasiliana na Tume ya Ubora na Usalama wa Utunzaji wa Wazee kwenye 1800 951 822 au angalia agedcarequality.gov.au. Huduma za Ukalimani zinapatikana.